

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA AROBAINI NA TANO**

**11 JUNI, 2024**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA TANO TAREHE 11 JUNI, 2024

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**578. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaipa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Katibu Muhtasi.

**579. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kuweka zege kwenye Barabara za Mlimani Jimbo la Same Magharibi ili kuokoa gharama za kuweka vifusi mara kwa mara.

**580. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Shule ya Wasichana Arusha ambayo ilipangwa kujengwa katika Kata ya Enkikret - Longido.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**581. MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni Mikataba mingapi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi ambayo Watumishi wake wanatoka Zanzibar.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA  
YA HABARI:**

**582. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL  
ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,  
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Kata za Bwakila Juu, Singisa pamoja na  
Mkulazi Morogoro Vijijini zitapatiwa Mawasiliano ya  
uhakika.

**WIZARA YA MAJI:**

**583. MHESHIMIWA SILYVESTRY FRANCIS KOKA  
(KIBAHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha Mamlaka ya  
Maji Mkoa wa Pwani ili kuondoa changamoto ya  
maji maeneo mengi ya Mkoa huo.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**584. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA  
(KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi  
na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha Ufundi VETA katika Mji wa Ifakara.

**WIZARA YA KILIMO:**

**585. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Makampuni gani yalishiriki ununuzi wa Kahawa Mkoani Kagera kwa Mwaka 2023.

**WIZARA YA AFYA:**

**586. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha Afya Vwawa.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**587. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI (TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali italipa fidia au kurejesha maeneo ya Wananchi katika Mlima Nkongore yaliyochukuliwa na Jeshi la Magereza – Tarime.

#### **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

##### **588. MHESHIMIWA TAMIMA HAJI ABASS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itatunga Sheria mahsusi kwa makosa ya ukatili wa Kijinsia.

##### **589. MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX (BUHIGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya ya Buhigwe ili Wananchi waweze kupata huduma.

#### **WIZARA YA FEDHA:**

##### **590. MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE RUHORO (NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Forodha cha Mugoma.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**591. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, mpango wa ujenzi wa Reli ya Kusini umefikia hatua gani.

**DODOMA  
11 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**

